

## Maswali

1. Nani alikuwa baba wa Daudi.
2. Daudi alikuwa na ndugu wangapi? Ndugu wake walikuwa wapi?
3. Kazi ya Daudi ilikuwa nini?
4. Daudi alifanya nini alipokuwa akichunga kondoo?
5. Daudi alitumia nini kurudisha kondoo waliotanga tanga tena ku-wapiga wanyama wa mwituni?
6. Mbona Daudi hakuogopa?
7. Mnyama gani alishambulia kondoo na akachukua mwana kondoo?
8. Daudi alifanya nini?
9. Daudi aliua mnyama gani mwingine wa mwituni?
10. Mbona Mungu alisaidia Daudi?

## Majibu

1. Jese alikuwa baba wa Daudi.
2. Daudi alikuwa na ndugu 7. Walikuwa wanapigana kwa jeshi la Sauli.
3. Daudi alichunga kondoo wa baba yake.
4. Daudi alicheza kinubi na alitunga nyimbo za kumsifu Mungu.
5. Daudi alitumia kombeo na mawe.
6. Daudi hakuogopa kwa sababu aliamini Mungu.
7. Simba alishambulia kondoo.
8. Daudi alifuata simba, akashika ndevu yake na kumua.
9. Tena Daudi aliua dubu.
10. Mungu alisaidia Daudi kwa sababu alimwamini.

## SHULE YA JUMAPILI YA CBM

**Awamu ya 1 Mwaka wa 3**



# 26 Daudi mchungaji kijana

## Marejeo

1 Samweli 17: 34 – 35 na Zaburi 23

## Kiini cha somo

Kuonyesha kwamba Daudi aliamini Mungu wakati alikuwa kwa shida au kwa hatari, na Mungu alimsaidia.

## Maneno maalum

- 26.1 Daudi + mwana mdogo + kondoo + penda Mungu
- 26.2 Daudi + muziki + kinubi + nyimbo + sifu Mungu + Zaburi
- 26.3 Daudi + jasiri + kombeo na mawe + kondoo tanga tanga + wanyama wa mwitu + amini Mungu
- 26.4 Daudi + lisha kondoo + simba + shika mwana kondoo + Mungu saidia + ua simba + ua dubu
- 26.5 Daudi + maisha tulivu + penda uvumbuzi + amini Mungu

**26.1** Daudi alikuwa ndiye mdogo kwa wana wa Jese wanane. Ndugu wa Daudi wakubwa walikuwa kwa jeshi la Sauli wakipigana na Wafilisti. Lakini

Daudi alikuwa bado mtoto hangeweza kwenda kwa vita. Alichunga kondoo za babake.




Daudi alifurahia sana kukaa nyumbani na kuchunga kondoo. Alipenda Mungu sana. Alifurahi kukaa kwa utulivu kwa nyasi kando ya vilima akiomba Mungu na kumshukuru kwa kila kitu alichofanya.

**26.2** Daudi alipenda muziki. Alipiga kinubi wakati alikuwa akichunga kondoo. Alitunga nyimbo nyingi za kumsifu Mungu. Aliunda sauti kwa kinubi na kuziimba kama nyimbo. Wimbo moja wa Daudi ni Zaburi 23.



**26.3** Daudi alikua mjasiri na alipenda uvumbuzi wa vitu. Alitazamia wakati atakapoenda vitani ili apiganie jeshi la watu wa Mungu. Daudi alitumia kombeo na mawe. Alirusha mawe kwa kombeo ili arudishe kondoo waliotanga tanga na kwenda kando. Alitumia kombeo na mawe kuua wanyama wa mwituni

na kuwatisha wawachane na kondoo. Kila siku alijifunza kutumia kombeo na mawe. Mpaka alikuwa hodari wa kutumia kombeo.



Daudi aliamini kwa Mungu na kila mara alifuata amri za Mungu. Alijua kwamba hatakiwi kuwa na uoga kwa sababu Mungu alikuwa akimlinda. Alikumbuka Mungu wakati alikuwa msituni na kwa mito.

**26.4** Siku moja, Daudi alikuwa amekaa chini ya mti ameangalia kondoo wakila nyasi. Kwa ghafula aliruka juu. Simba alikuwa ananyemelea ili amrukie kondoo mmoja.

Daudi alipojaribu kuruka juu, simba alishika kondoo kwa mdomo wake na kwenda. Daudi hakuogopa, alijua Mungu atamsaidia. Alifuata huyo



simba. Alipiga simba na akatoa kondoo kutoka kwa mdomo wake. Simba aligeuka na kutaka kumshambulia. Daudi alishika huyo simba kwa kidevu na kumua. Tena aliuwa dubu aliyetaka kuiba mwana kondoo mmoja.

**26.5** Ingawaje Daudi alipenda maisha yaliyokuwa tulivu, alipenda kuvumbua pia. Daudi aliamini Mungu wakati wote na Mungu alimsaidia.